# MAHUSIANO 103

## NAMNA YA KUENENDA KATIKA UCHUMBA

JAMES KALEKWA

# MAHUSIANO 103:

*Namna ya kuenenda wakati wa uchumba.*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo


1. Ujenzi ........................................................................ 4

   Mzizi wa fikra duni: ........................................................ 5

      Malezi:.................................................................. 6

      Marafiki/Kundirika: .................................................. 7

      Kisa cha macho makubwa:........................................... 8

   Kijana wa kiume kumuelekea binti: ................................. 8

   Binti kumuelekea kijana wa kiume: ................................. 9

2. Ulinzi na Usalama ....................................................... 10

3. Uhakikisho ................................................................. 12

4. Usafi ......................................................................... 15

5. Kuwa kielelezo kwa vijana wengine ............................ 18

6. Mazungumzo magumu ................................................ 20

*“Mimi ni ua la uwandani, Ni nyinyoro ya mabondeni.”* **Wimbo Uliobora 2:1**

Mahusiano yameanza baina ya kijana [Sulemani] na binti Mshulami; kila mmoja kajipatia dhahabu yake katikati ya mchanga. Swali kubwa la kujiuliza ni maisha yanafananaje kabla ya kuingia kwenye ndoa; nini kinafanyika hapa.

Nimekuwa mchungaji wa vijana kwa muda kiasi na mshauri wa vijana kwa muda mwingi kiasi; moja ya jambo ambalo huwa linajitokeza ni hali kujisikia kutotosha kuwa mwenzi wa mtu fulani. Ni kama vile kuna vigezo vinapungua kwako au hukustahili.

Neno la Mungu linatoa mwongozo namna ya kuiendea safari hii.

## 1. Ujenzi

Andiko linalotufungulia ukurasa hapa [Wimbo Uliobora 2:1] ni mwendelezo hisia za uduni na kutostahili zilizokuwa ndani ya binti. Anajifananisha na ua la uwandani. Si kwamba anajisifia au anaona ufahari ya kwamba yeye ni ua, la hasha! Bali anajiona ni wa kawaida tu.

Ukisoma tafsiri za lugha ya kiingereza utaona anachokinaamisha.

“I *am* ***merely*** *a rose* from the land of Sharon, a lily from the valley.” CEV

“I am ***just a wildflower picked from the plains*** of Sharon. A lotus blossom from the valley pools.” Message

“I am a rose ***[of the plain]*** of Sharon, The lily of the valleys [the grows in deep places]” AMP

Ukisoma kwa umakini utagundua ya kwamba ya kwamba binti alikuwa anasema *“mimi ni mtu wa kawaida sana; mimi ni mtu wa shamba/mabonde kuinama”… just a wildflower; a rose of the plain; merely a rose!* Yeye si lolote si chochote.

Kuna tofauti kati ya unyenyekevu na uduni… ukifuatilia vizuri huu ni uduni. Ni changamoto kubwa sana kuingia kwenye ndoa na mwenzi ambaye anaona umemfanyia hisani [huruma] kuwa naye kwenye uchumba; na vilevile si sawa kujiona wewe ni bora kuliko mwenzi wako. Ni kama vile umemfanya tendo la msaada kuwa naye kwenye uchumba huo.

### Mzizi wa fikra duni:

Huyu binti hajaanza leo kujiona duni. Hkuanza leo kujiona yeye ni wa “mabonde kuinama”. Ukisoma vyema sura ya kwanza ya Wimbo Uliobora utaona wazo hili lilikotokea.

Malezi:

“”Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. *Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda*.” **Wimbo Uliobora 1:5**

Wazo hili la kutofaa alilipata nyumbani kwao; kaka zake wa kufikia [wana wa mamangu] walimkasirikia na kumuweka ashinde kutwa kwenye mashamba ya mizabibu akifanya kazi ya ulinzi. Biblia haisemi baba yake alikuwa wapi wakati hayo yote yanatendeka; Biblia haizungumzi chochote kuhusiana na mwitikio mama yake kwa tabia za wana [sons] wake kumtenda dada yao kwa uonevu hivyo.

Lakini matokeo yake akawa mweusi-mweusi; hakulilinda shamba lake.

Wakati wa uchumba ndiyo kipindi ambacho utaanza kuona matokeo ya malezi aliyokulia mchumba wako.

Inawezekana anatokea kwenye ndoa iliyovunjika; ndoa ya mitala; malezi ya mzazi mmoja; wazazi wakatili; uonevu wa kaka [ndugu] zake.

Matokeo yake anakuwa mtu aliyejaa uchungu, hasira, kisasi, kujisikia duni na kutofaa. Haya yote ni mambo unapaswa kushughulika nayo wakati wa uchumba.

Marafiki/Kundirika:
"5. Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, *Enyi binti za Yerusalemu.* Mfano wa hema za Kedari, kama mapazia ya yake Sulemani. 6. *Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi*…." **Wimbo Uliobora 1:5-6a**

"… kwa hiyo *wanawali* hukupenda" **Wimbo Uliobora 1:3b**

Kuna hili kundi ambalo linaitwa "wanawali" na mahali pengine analitaja kama "Binti za Yerusalemu". Hawa ama ni rafiki zake au ni watu wa umri sawa na yeye [kundirika]. Unaona si tu kwamba wanapenda kuwa na mahusiano na kijana yule bali wanaenda mbali na kuanza kumchunguza-chunguza mwenzao. Na uchunguzi wao huo ni wa kumtoa kasoro na kumwonyesha namna gani asivyofaa au kustahili kuwa mchumba wa yule kijana wa kiume.

Ulisoma Kitabu cha Mahusiano 102? Kuna kipengele ambacho nimeonyesha taswira ambayo hujengeka mawazoni mwangu kila nisomapo andiko hili. Rudi tena ukisome!

Kwenye mazingira yetu hawa ni aina ya watu wanaopenda kukudhihaki au kukutania [bullying]. Moja ya matatizo makubwa sana ambayo hayasemwi sana kwenye jamii ni hili tatizo la *"bullying"*. Watu wengi wamekuwa *"bullied"* shuleni, vyuoni, mitaani na kwenye makazi yao. Mara nyingi ni kutoka kwa

wanakundi-rika [agemates] au watu wanaokua nao [contemporaries].

Hii imezalisha hisia za uduni, unyonge, kutostahili… imefifisha kujiamini.

Kisa cha macho makubwa:
Mimi, James Kalekwa, ni muhanga wa "bullying". Ni kweli Mungu ameniumba kwa namna ya ajabu na ya kushangaza kwa kunipatia macho makubwa. Lakini kuna wanakundirika wangu walinisema vibaya wakati ninakua. Kiasi kwamba ilinipotezea kujiamini au kusimama mbele ya watu. Siku moja mke wangu (tukiwa wachumba bado) aliniambia, "James, una macho mazuri sana. Na huwa ukiongea, yanakusaidia kuongea pia…" Badala ya kushukuru, nilimkasirikia sana. Ilichukua muda kumsamehe! Hata hivyo, alitumia muda kunisaidia kuelewa alichomaanisha. Na tangu wakati huo nikapokea uponyaji kamili kabisa. Na sasa, ninamtukuza Yesu kwa ajili ya macho makubwa. Bwana asifiwe!

Ikitokea umebaini kwa mchumba wako hali hii ya kujiona yeye ni "ua la uwandani au nyinyoro ya mabondeni" basi kumbuka kufanya UJENZI!

## Kijana wa kiume kumuelekea binti:

"Kama *nyinyoro kati ya miiba*, Kadhalika mpenzi wangu kati ya mabinti" **Wimbo Uliobora 2:2**

Kijana wa kiume anaanza kufanya mambo ya kiume hapa. Kumjenga mchumba wake kwa maneno. Anamwambia kama wewe [mpenzi wangu] ni nyinyoro basi mabinti wengine ni miiba! Wewe ni bora sana kuliko wao, ndiyo maana nilikufuata wewe.

Kijana wa kiume, usimdidimize mchumba wako pindi anapoonyesha kujisikia dhaifu au duni. Badala yake tumia kinywa chako kumjenga na kuonyesha msimamo wako kumuelekea.

Binti kumuelekea kijana wa kiume:
"Kama *mpera kati ya miti ya msituni*, Kadhalika mpendwa wangu kati ya vijana." **Wimbo Uliobora 2:3**

Ajabu na kweli, moyo uliojengwa na kuhakikishiwa unapendwa. Nao huitikia kwa ujenzi na pendo jingi. Binti anamjibu kijana na kumwonyesha yeye ndiyo "mpera" na vijana wengine wote ni "miti ya msituni".

Binti, usiishie kuwa mpokeaji tu wa maneno ya ujenzi, bali nawe jitoe kumjenga mchumba wako kwa kutumia kinywa chako.

Neno la Kristo husema hivi;

*"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi,*

*na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."* **Wakolosai 3:16**

Ninaomba kutambulisha kwako kifaa cha ujenzi kinachoitwa neno la Kristo.

Kumjenga mchumba wako si kumtamikia maneno ya ulaghai au kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Ni kumwambia neno unaloliamini sana ndani kumuhusu. Na hilo linapaswa kuwa neno la Kristo.

## 2. Ulinzi na Usalama

"Naliketi *kivulini mwake kwa furaha*, Na matunda yake naliyaonja kuwa matamu." **Wimbo Uliobora 2:3b**

Unakumbuka huyu binti ametumia sehemu kubwa ya maisha yake [walau tunayoonyeshwa na maandiko] kwenye mashamba ya mizabibu kama mlinzi? Unakumbuka? Na kwa kinywa chake mwenyewe anatuonyesha ya kwamba "amunguzwa na jua."

Hata hivyo, baada ya kukubali kuwa mchumba wa kijana huyu, moja ya jambo analokutana nalo ni **kivuli** na **furaha**.

Kwanza, inaweza kumaanisha ni kivuli tunachokifahamu au kuna lugha ya picha. Mimi ninapendelea zaidi kutazama kama lugha ya picha. Namaanisha kuna utulivu, pumziko, hewa safi na

matulizo ya nafsi ambayo anayapata kwa kuwa mchumba wa huyu kijana.

Unakumbuka malezi ambayo binti huyu amekulia? Kukasirikiwa na wana [sons] wa mama yake na kutupwa shambani kama mlinzi. Upande mwingine ni wazazi kuwa kimya na kutochukua hatua yoyote.

Kwa ufupi, huyu binti hajawahi kuona wanaume wanaopenda.

Bwana akamkutanisha na muujiza wake. Akatulizwa kivulini.

Na anenda mbali zaidi kutuonyesha jinsi pendo la kijana yule wa kiume lilivyo zuri. Kwa kimombo kuna usemi *"second to none".* Ndivyo anavyofafanua binti.

*"Na matunda yake naliyaonja kuwa matamu."* 2:3b

Kijana wa kiume unayesoma hapa, hakikisha mchumba wako anayasema haya kukuhusu wewe; Siyo binti wa watu aanze kujihisi kubakwa, kushikwashikwa, kuvunjiwa heshima na/au kuchezewa anapokuwa na wewe. Tena binti wa namna hii ambaye ametokea kwenye mazingira yaliyomuumiza, usimuongezee maumivu kwa kumtenda hiyana. Mlinde na umuhakikishie usalama wake. Anapaswa kujua, mikononi mwako ni sehemu salama. Atapata kivuli na furaha; atafurahia utamu wa matunda [pendo] yako.

Hata kama binti mwenyewe atataka kukuingiza kwenye mtego wa namna hiyo. Hakikisha unamlinda. Ni kwa usalama wenu! Uchumba si sehemu ya *“kubanduana”;* mna mambo mengi ya kushughulika nayo.

Mabinti wataafikiana na mimi ya kwamba kuna “wakaka” ambao wakikaa nao huwa hawajisikii salama. Unahisi kama utabakwa au kishikwa isivyo kwa heshima dakika yoyote ile.

Mwanamume, hakikisha unamlinda binti. Wewe ndiye mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama hapo. Ongoza shughuli ya ulinzi!

## 3. Uhakikisho

“Akanileta mpaka nyumba ya karamu, Na bendera yake juu yangu ni mapenzi.” **Wimbo Uliobora 2:4**

Kwenye muktadha wa utamaduni ambamo Kitabu hiki kimewandikwa, inaonekana kulikuwa na nyumba kadhaa kutegemeana na matumizi ambazo mtu alikuwa nazo kulingana na uwezo wake. Na hapa tunatambulishwa ya kwamba kumbe kijana likuwa na “nyumba ya karamu”

Kwa faida yetu pamoja, ni vizuri tukaelewa ya kwamba kwenye karamu watu hualikwa. Hakuna mtu hujiendea kwenye karamu bila mwaliko (Yohana 2:2/Mathayo 22:3). Ndivyo ilivyo kwenye mazingira yetu, kuna kadi za mwaliko na kuna walinzi mlangoni ambao hukagua kadi.

Tutakubaliana pia mwaliko wa kuhudhuria karamu huamuliwa na kiwango cha mahusiano. Huwezi kuleta watu usiowafahamu kwenye karamu yako! Hivyo basi, ukitaka kuwafahamu ndugu zangu, njoo kwenye nyumba yangu ya karamu.

Hiki ndicho alichokifanya kijana wa kiume. Baada ya kuwa na mahusiano baina yao binafsi [yeye na binti]. Akaamua kwenda hatua kubwa zaidi ya kumpeleka binti "kwa watu wake wake ndani" – kwenye nyumba ya karamu. Huu ulikuwa ni utambulisho. Unaweza ukawa si ule utambulisho rasmi, lakini hakukaa kimya na mahusiano haya. Aliwafungukia watu wake wa karibu.

Mahusiano si kama biashara haramu, uhalifu au jambo ovu lolote. Hayapaswi kukaa mafichoni. Yanapaswa kujulikana haraka iwezekanavyo kwa watu wa "nyumba ya karamu". Hii huonyesha ni kwa kiasi gani mmemaanisha. Na hili ni kwa usalama wenu wote wawili.

“Nyumba ya karamu” hufanyika ukuta wa ulinzi kwenye mahusiano yenu ikitokea mmoja wenu analegalega na kukengeuka.

Kwenye lugha ya Kiswahili kuna neno linatumika “bendera”; na kwenye tafsiri za kiingereza zinasomeka "banner" ambayo ninaweza kuitafsiri kama bango.

Umewahi kuona bango la mkutano wa injili? Umewahi kuona bango mbele ya kanisa limeandikwa “Yesu yuko hapa” au “Yesu ni Bwana” au “Yesu ni yule jana, leo na hata milele.”? Haya mabango huwa yanafichwa? Au yanawekwa chini-chini? Je, huwa yanaandikwa kwa mkwaruzo? Umewahi kuchunguza machagua ya rangi zake?

Iko hivi, bango huwa halifichwi, kuwekwa chini, au kuandikwa kwa maneno yaliyofifia na machagua ya rangi zake ni rangi zinazoonekana kwa urahisi na kuvutia msomaji. Bango siyo siri!

Sasa, binti anatuonyesha ya kwamba “Na bendera [bango] yake juu ya mapenzi.” Kijana ameamua kuweka mambo yote hadharani. Ni ameamua kuutangazia ulimwengu *“Mimi kijana XYZ nimeamua kumpenda binti ABC.”*

Uchumba ujulikane. Vijana [wa kiume na wa kike] msipendelee kuwa na uchumba bubu. Haitakuwa kwa

faida yenu kwa namna yoyote ile. Mara nyingi, hupelekea maumivu.

Kama unampenda, chonga bango!

Kma unampenda, acha nyumba yako ya karamu na ijue… acha dunia na ijue!

Kutoijulisha nyumba yako ya karamau, na kutochonga bango huwa ni kiashiria cha "nia ovu" moyoni mwako.

## 4. Usafi

*"Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vyema yenyewe."*
**Wimbo Uliobora 2:7**

Mapenzi huwa yanachochewa; mapenzi huwa yanaamshwa!

Nikiwa kijana mdogo wa miaka kumi na tano hivi [15] nilipewa zawadi ya kitabu cha mtheolojia (wakati huo) Rev. Mkumbo G. Mitula kiitwacho "Chokochoko la Mahaba". Usihofu kuhusu jina la Kitabu. Mwandishi ni mtumishi wa Mungu kabisa. Kundi la watu alilolenga kulifikia angelifikia kwa jina kali namna hiyo.

Kule ndani anafafanua dhana ya kuyaamsha mapenzi. Anatumia mfano [allegory] ya kumwamsha mtu.

Mtu aliyelala haamshwi kwa namna yoyote ile. Huwezi kwenda na kumpigia kelele tu, au kumwita kwa sauti; si vyema kumwamsha kwa kumpiga ngumi au kibao, au kumwagia maji. Ni kweli unaweza ukafanya hivyo, lakini madhara yake ni makubwa. Mtu huyu anaweza kushtuka kutoka usingizini na kuanza kufanya mambo ya ajabu. Anaweza kuinuka na kuendeleza kwenye uhalisia kile alichokua anakiota ndotoni, mwingine anaweza kukimbia hovyo na wengine hata huzirai hata kupoteza uhai.

Kwanza, kiasili, Mungu ameweka namna ambayo mtu mwenyewe "hujiamsha" kutoka usingizini na kuwa macho. Na jambo hili la asili hufanyika bila jitihada wala maumivu yoyote. Limewekwa na Mungu ndani yetu. Huhitaji kujitahidi; muda wa kuamka ukifika, unaamka tu.

Pili, ikitokea ni lazima sana mtu aamshwe kutoka usingizini. Ni vizuri kumwamsha mtu usingizini *"sanaa na sayansi"*. Kuna namna ya kumgusa na maeneo ya kumgusa kwa utaratiu ili aamke.

Kwa mfano huo, binti Mshulami nawaambia wenzake *"msiyachochee wala kuyaamsha mapenzi, hata yatakapoona vyema yenyewe."* Akimaanisha, mapenzi na vionjo vyake, ni zawadi na baraka kutoka kwa Mungu. Kuna mwenendo wake ambao Mungu

ameyawekea ndani yetu. Muda utafika, yataona vyema yenyewe, yataamka!

Anayesema hivi, ni mtu ambaye yumo ndani ya mapenzi; ni mtu ambaye anasema kutokea kwenye moyo wa shukurani [si majuto]. Anashukuru ya kwamba alikutana na kijana ambaye si "mchochezi wala mwamshaji". Kijana ambaye amekubali kuacha mapenzi yatiririke yenyewe kufuata mkondo wake hali wao wakishughulika na mambo ya msingi.

Isingekuwa rahisi kwao kuwaasa wenzao iwapo wangekuwa wamepita njia ya "kuchochea na kuamsha".

Jamii tuliyonayo ni mahali ambapo swala la mapenzi linachochewa na kuwashwa kwa nguvu sana. Ni jamii iliyochemka kweli kimapenzi. Vijana wamewaka haswa. Mazungumzo ya mapenzi, nyimbo za mapenzi, michoro ya mapenzi, matangazo ya mapenzi, video za mapenzi… utulivu hakuna! Kuna vijana wengi sana wameamka kimapenzi, ukisikiliza unagundua wanaota huku wanatembea. Ni wengi wameamshwa kwa kumwagiwa maji usoni au kuchapwa kibao.

Mapenzi na vionjo vyake ni nishati [energy] ambayo ni zawadi na baraka kutoka kwa Mungu. Nishati zote huwa na tabia moja – kama vile maji au umeme. Visipowekewa mkondo mahususi wa kupita, huwa na vurugu [violent] na kuleta madhara.

Kwenye uchumba si sehemu ya kuamshana na kuchocheana kimapenzi. Madhara yake ni makubwa sana. Tumieni muda wa uchumba kuweka misingi mizuri ya ndoa. Na zaidi ya hapo binti Mshulani, anataka wenzake wajue ya kwamba "Usiyaanzishe kama hauna mpango wa kuyatimiliza."; Ni kama anawaambia, "kama huna uhakika na mwisho, usianze."

Vijana wengi wamechanganyikiwa na manarukaruka kama kuku aliyekatwa kichwa kwenye eneo hili la mapenzi kwa kuwa hapo awali walianza safari hii ya mapenzi bila kujua hatima yake. Wakajikuta wameshushiwa njiani. Wamepotea; hawajui wanarudi vipi mwanzo; na hawajui wanaelekea vipi mbele.

## 5. Kuwa kielelezo kwa vijana wengine

Mimi na mke wangu ni wazaliwa wa kwanza kwenye familia zetu; Moja ya jambo tulilojifunza mwanzoni kabisa mwa maisha yetu ni kwamba wazee wanamatarajio makubwa na sisi; na ndugu zetu wanatutazama kama kielelezo. Iwe kwa kujua au kutokujua; kwa kukusudia au la, ndugu zetu watatutazama na watafuata kile tunachokiishi kama mfano.

Jambo hili lilitupelekea kuanza kuchonganidhamu fulani kwenye maisha yetu. Kuna mahali ambapo hatutenda kwa ufasaha sana au kwa kiwango kilichotakikana – tulipungukiwa na utukufu. Lakini ninachosema ni hiki, unapaswa kujua ya kwamba kuna watu wanakutazama.

*"Nawasihi, **enyi binti za Yerusalemu**, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, hata yatakapoona vyema yenyewe."*
**Wimbo Uliobora 2:7**

Unaona binti huyu. Kuna watu wa umri wake/kundirika, watoto wa mjini, ambao hapo awali walikuwa kinyume naye. Lakini baada ya kufahamika kwa uwazi, yeye ndiye "mama mtumishi", hawi na kinyongo. Bali yale anayojifunza kwenye maisha yake, anawarushia na wao kama madarasa – anawafundisha na kuwa kielelezo kwao.

Baadaye kwenye safari ya maisha, mimi na mke wangu tukagundua kuna watu kadhaa ambao wanatufuatilia na kujifunza kwetu. Hii ilitupa kuweka bidii kuwa watu bora na wa thamani zaidi.

Mara kadhaa huwa tunakumbushana, kama tunadhani tumechoka kuenenda vyema kwa ajili yetu na faida yetu wenyewe basi tujiangalie sana tusiwakoseshe na wengine; tuenende vyema kwa faida ya wengine! Kila

tukikumbuka kuna kilelezo tunakiweka, jambo hilo hutunyenyekeza na kutuhimiza sana.

Kijana [wa kiume na wa kike], iwe unajua au haujui; unapenda au haupendi – unawajibika kimaadili kwa watu wanaokufuatilia ambao unapaswa kuwa kielelezo kwao. Chunga hatua zako [mind your steps].

## 6. Mazungumzo magumu

“Tukamatieni mbweha, Wale mbweha wadogo, waiharibuo mizabibu, maanza mizabibu yetu yachanua.” **Wimbo Uliobora 2:15**

Mizabibu imechanua; Penzi linakua. Penzi linajengwa kwa kukusudia, hakuna hata kimoja kilichotokea kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi.

Kama mwandishi, ninataka uone lugha ya nafsi ya kwanza wingi [Pole kama Kiswahili kinasumbua] inavyotumika hapa “Tukamatieni” kisha angalia “mizabibu yetu”. Haya maneno hayatokezi kwa bahati mbaya. Bali yanaelezea hali ya mioyo na mahusiano ya wachumba hawa. Ni uchumba uliojengwa ukajengeka.

Pia, ninataka uone kuna “mbweha wadogo” ambao kazi yao ni kuharibu mizabibu inayochanua.

Usisahau binti amewahi kuwa mlinzi wa mashamba ya mizabibu. Kwa hiyo anatumia lugha na uzoefu wa maisha kujenga uchumba wao.

Mbweha wadogo – nani anawaogopa? Nani anawatilia maanani? Wanaweza kufanya nini?

Ni mambo madogomadogo usiyoyadhania; vijitabia vyako na/au vyake; mitazamo kadhaa juu ya mambo ya maisha; hulka zako/zake; mwenendo na mtindo wa maisha; namna unavyochukulia mambo. Hao ni mbweha wadogo.

Haya ni mazungumzo ambayo mtaenda ndani na kushughulika na maswala ya fedha [fedha ni za nani? zako, zangu, zetu]; namna ya kutatua migogoro; kushughulika na hasira; majukumu ya nyumbani; maswala ya mavazi; nini kikitokea ndoa hii itavunjika? Na mambo yanayofanana na hayo.

Ushindi dhidi ya hasira:

Nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa 3 chuoni [2011] (st. Augustine University of Tanzania) nilikuwa ninashiriki jumuiya ya Kikristo ya wanafunzi wa vyuoni inayofahamika kama USCF. Tulikuwa na mahafali ya jumuiya pale chuoni, na mchumba wangu [mke wangu sasa], Frida alikuwa anaishi na kufanya kazi Dar es Salaam. Hajawahi kunitembelea kabisa Mwanza. Nikamsihi na kuomba sanna, alikubali kuchukua likizo ili ahudhurie mahafali hayo – tuonane!

Alipofika Mwanza, nilimpokea na kumpeleka kwa dada zangu na rafiki zangu wa fellowship [Rosterbella na Grace] akafikia kwao na kuishi hapo.

Jioni moja [siku moja kabla ya mahafali], nilimuomba tunane chuoni kuzungumzia jambo fulani. Alifika na tukawa kwenye mazungumzo, hata hivyo mazungumzo yetu yaliharibika. Tulishindwa kukubaliana juu ya jambo tulilokuwa tukizungumza. Mimi nilijiona niko sawa na sikuelewa kwa nini alikuwa haoni pointi/kile ninachomaanisha. Nilijaribu kumfikirisha kwa namna nyingi, bado hakukubaliana na mimi. Ilikuwa ni mazungumzo kuhusu maisha baada ya kuhitimu chuo; na majadala ulifikia kuzungumzia juu maswala ya utumishi na kufanya kazi/ajira.

Niliumia sana kwanini hanielewi, tulikuwa mahali pa wazi. Sikutaka kuongea kwa sauti iliyopazwa. Niliinuka na kubamiza kwa nguvu sana simu yangu ya mkononi chini – kwa hasira. Nilitetemeka, niliogopa nilichokifanya; na Frida aliogopa sana. Hajawahi kuniona nikiwa hivyo. Alishangaa! Akanisaidia kuokota mabaki ya simu na “line”. Lakini bado niliuona mshangao na uoga kwenye macho yake.

Tukaagana na kukubaliana swala hilo tutalizungumza baada ya mahafali. Kwa sasa, tuendelee na mahafali kwa furaha tu [tuna utaratibu tuliojiwekea juu ya

kutatua migogoro. Ya kwamba unaweza kumuhakikishia mwenzako upendo hata kama amekukosea, na tutaongea wakati mwingine juu ya kosa hilo].

Baada ya mahafali tulikutana na “mshitakiwa” nilikuwa na kesi ya kujibu. Aliniambia kwa kifupi sana “Jimmy, sidhani kama tunaweza kuoana ukiwa ni mtu wa hasira namna hii; sijioni nikiwa salama. Hebu jiulize tungekuwa peke yetu ndani, tumeoana ni kitu gani kingenitokea? Sidhani kama uko tayari kuwa baba ukiwa na hasira namna hii, si utavunja watoto?” Niliendelea kusikiliza nikisomewa “mashitaka” kwa upole sana. Unajua mtu anapokueleza jambo la ukweli hata akiwa kwenye hali ya utulivu [composed] sana. Huwa inauma zaidi!

Niliumia, nilijutia. Lakini haikutosha. Nilimuomba Frida anisaidie tufunge safari pamoja ya kushinda hali ya hasira na “reactions” zisizo sahihi.

Ilikuwa ni safari ya maombi, mifungo, vilio mbele za Bwana, kusikiliza mafundisho…. Na siku moja nikasikia tu kwenye mazungumzo ya simu “Jimmy, nafikiri nimeona badiliko. Sasa tunaweza kuendelea na safari yetu ya kufunga ndoa na kuwa na watoto.”

Mungu si Kalekwa, mwaka 2013 tulifunga ndoa!

Nimetumia ushuhuda wetu kukuonyesha “mbweha wadogo” wanavyoharibu mizabibu. Na kukuonyesha namna **mazungumzo magumu** hufanyika! Msiigize kwamba hakuna mbweha wadogo; na wale msirohoshe ya kwamba hawapo.

Uchumba ni sehemu nyeti sana. Tumieni muda huo vizuri.

Mbweha wadogo, wakila mizabibu inayochipua baada ya muda hukua. Madhara ya mbweha aliyeachwa mpaka akakua ni makubwa sana.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: [https://www.newvinechurch.or.tz](https://www.newvinechurch.or.tz)

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764